**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

**DIVISHENI YA KAZI**

**DAR ES SALAAM**

**MAREJEO NA. 390 YA 2022**

(Kutokana na Uamuzi wa Tume ya Usuruhishi na Uamuzi – Kinondoni katika Mgogoro wa Kikazi Na.CMA/DSM/ILA/298/2022 mbele ya Mollel B.L. Msuruhishi wa tarehe 04/10/2022)

**KATI YA**

**JOSEPHINE SHIRIMA ...................................... MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**SUNHERALEX CONSULTING ............................. MJIBU MAOMBI**

**HUKUMU**

28/3/2022&25/4/2022

**OPIYO, J**

Mwombaji, Josephine Shirima ameleta maombi haya akiomba kurejewa kwa mwenendo ili kuweza kutengua uamuzi mdogo uliotolewa na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (Tume) katika mgogoro wa kikazi wenye Na. CMA/DSM/ILA/298/2022 ili kujiridhisha na uhalali wake wa kisheria, kimantiki, kimuktadha na kiuhalisia.

Historia ya mgogoro huu kwa ufupi ni; mleta maombi aliajiliwa na mjibu maombi kwa mkataba wa miaka miwili ulioanza tarehe 10/07/2017 na kutakiwa kuisha tarehe 10/07/2019 katika nafasi ya afisa masoko.

Mkataba huo ambao ulikuwa ukiendelea hadi tarehe 22/03/2022 pale aliposimamishwa kazi. Mleta maombi hakuridhika na kuufikisha mgogoro wa kikazi Tume tarehe 30/05/2022 kwa maombi ya nyongeza ya muda ambayo yalitupiliwa mbali. Mleta mamobi pia hakuridhika na ndipo alipofikisha maombi ya marejeo Mahakamani hapa.

Maombi haya yameletwa Mahakamani hapa yakiambatanishwa na hati ya kiapo cha mleta maombi, sababu za maombi haya za kisheria zikiwa:

a. *Endapo mleta maombi alishindwa kueleza sababu za msingi za kuweza kuongezewa muda.*
b. *Endapo msuluhishi alishindwa kutumia mamlaka aliyonayo kwa mujibu wa sheria.*
c. *Endapo Tume ilikuwa na mamlaka ya kusikiliza mgogoro wa msingi baada ya kuongezewa muda.*
d. *Nini stahiki na haki ya kila upande.*

Mleta maombi aliwakilishwa na Bwana Towa Selemani Bilali, mwakilishi binafsi, huku mjibu maombi akikosa kufika Mahakamani baada ya kupatiwa wito wa Mahakama kwa kukataa kupokea wito wa Mahakama kupitia kwa meneja wa kampuni, maelezo yaliyoandikwa na mjumbe wa shina kwa wito ulipolekwa na afisa wa Mahakama Bwana Fredy Ndimbo.

Hivyo, mjibu maombi alijikosesha haki yake ya kutoa utetezi wake Mahakamani maombi yakaendelea upande mmoja. Na kwa amri iliyotolewa tarehe 28/03/2023 na Mahakama shauri likapangwa kusikilizwa kwa njia ya maandishi.

Bwana Bilali aliwasilisha kuwa mleta maombi aliajiriwa na mjibu maombi katika mkataba wa miaka miwili kuanzia mwaka 2017 hadi 2019, lakini mleta maombi aliendelea kufanya kazi kwa mjibu maombi hata pale mkataba huo ilipofikia mwisho kutokana na kuwepo muendelezo wa kiajira katika vigezo na masharti yaleyale yaliyokuwa katika mkataba.

Aliendelea kueleza kuwa, mgogoro kati ya mleta maombi na mjibu maombi ulitokea tarehe 22/03/2023 ambapo alisimamishwa kazi bila kuelezwa sababu wala kupewa nafasi ya kujieleza. Akafahamisha zaidi kuwa tarehe 30/03/2022 mleta maombi alilazimika kusafiri Kwenda Moshi kumuuguza mama yake na kurudi Dar es Salaam tarehe 25/05/2022 na tarehe 26/05/2022 alipata usaidizi wa uwakilishi kutoka Alin Law Care wa kuandaa na kuziwasilisha Tume tarehe 07/06/2022. Katika kusisitiza hoja yake alirejea kesi ya **Damari Watson Bijinja dhidi ya Innocent Sangano**, Miscellaneous Civil Application No. 30 of 2021, High Court of Tanzania - Kigoma.

Bwana Bilali aliendelea kuwasilisha kuwa uamuzi mdogo una makosa ya kisheria kwakuwa msuluhisi alitoa siku zisizo sahihi ambazo ni siku 77 wakati kiuhalisia ni siku 45 kuanzia tarehe 21/04/2022 (ambazo alikuwa na sababu za msingi) kwakuwa siku 30 za mwanzo zilipaswa kuisha tarehe 20/04/2022. Aliendelea kueleza kuwa tarehe 21/04/2022 mleta maombi alikuwa yupo Moshi akimuuguza mama yake hadi tarehe 25/05/2022 alipoanza safari ya kutoka Moshi kurudi Dar es Salaam.

Aliendelea kuwasilisha kuwa uamuzi wa mjibu maombi kumsimamisha mleta maombi kazi bila ya sababu wala kupewa nafasi ya kujieleza ni haramu kwani kinakiuka haki ya msingi ya binadamu kama ilivyoelezwa katika ibara ya 13(6)(a) ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kukazia hoja yake hiyo alirejea kesi ya **Andrew Athuman Ntandu na mwenzake dhidi ya Dustan Peter Rima (as an administrator of the estate of the late Peter Joseph Rima)**, Civil Application No. 551/01 ya mwaka 2019, Mahakama ya Rufaa ya Tanzania – Dar es Salaam na **Principal Secretary, Ministry of Defence and National Service Vs. Devram Valambia** [1992] TLR 182.

Aliendelea kuwasilisha kuwa, msuluhishi hakuzingatia hoja za mleta maombi za kumuuguza mama yake kwa kueleza kuwa hakuwalisisha vielelezo vya kuthibitisha ugonjwa. Kwa maoni ya mwakilishi wa mleta maombi ni kuwa mleta maombi aliwasilisha tiketi za basi zilizoonyesha kuwa mleta maombi alikuwa safarini ambazo msuluhishi hakuzizingatia.

Bwana Bilali aliwasilisha kuwa msuluhishi hakuzingatia kuwa mleta maombi hakuwa na njia nyingine yoyote ya kumuingizia kipato kuweza kugaramia utoaji wa taarifa ya tabibu inayohusu ugonjwa wa mama yake ambayo isingeweza kutoka kwa muda mfupi. Kwamba utoaji wa taarifa za mgonjwa una taratibu zake ili kuzingatia haki za mgonjwa zinalindwa. Mwakilishi wa mleta maombi alifahamisha kuwa mleta maombi asipopata haki ya kusikilizwa itamnyima stahiki zake za kiajira na kuwa hakuna hasara yoyote kwa upande wowote endapo maombi haya yatakubaliwa. Akawasilisha zaidi kuwa mjibu maombi hana nia ya kuyapinga maombi haya na ndo maana hajafika Mahakamani na hivyo akaomba maombi haya yaweze kuruhusiwa.

Baada ya Mahakama kupitia mawasilisho hayo imebaini kwamba hoja ya kuijibia ni kama mleta maombi alikuwa na hoja stahiki za kumwezesha kupewa ruhusa kufungua shauri nje ya muda. Ili kuweza kujibia hoja hii

inabidi kufahamu sheria inaeleza nini kuhusiana na ufunguaji wa migogoro ya kazi katika Tume. Kanuni ya 10(1) ya Sheria za Taasisi za Kazi (Usuruhishi na Uamuzi) T.L.S. Na. 64 ya mwaka 2007 inaelekeza kuwa mashauri ya migogoro ya kazi ya uachishwaji wa ajira yafunguliwe Tume ndani ya siku 30 tangu mgogoro huo ulipotokea ambapo mwajiri alifanya maamuzi yake ya mwisho ya kumwachisha kazi mwajiriwa.

Katika shauri hili nyaraka (CMA F1) inaonyesha kuwa mgogoro wa kazi baina ya mleta maombi na mjibu maombi ulianza tarehe 22/03/2022 na mleta maombi akafikisha mgogoro huo Tume tarehe 30/05/2022 ikiwa ni baada ya siku 69 tokea mgogoro huo wa kazi utokee. Pamoja na uhalisia huo Mahakama na Tume zina mamlaka kisheria kuruhusu migogoro iliyo nje ya muda kufunguliwa. Lakini mamlaka hayo yanatakiwa kutekelezwa kimahakama. Hii inamaanisha; ili muda wa kufungua shauri uweze kuongezwa ni lazima mleta maombi aonyeshe sababu za msingi zilizopelekea yeye kuchelewa kufungua maombi kwa wakati. Hayo yameelezwa katika mashauri mbalimbali ya Mahakama ya Rufani ya Tanzania; moja ya mashauri ni kati ya **Wambura N.J. Waryuba dhidi ya The Principal Secretary Ministry for Finance and Another**, Maombi ya Madai Na. 320/01 of 2020, Mahakama ya Rufaa ya Tanzania – Dar es Salaam.

Mleta maombi kupitia mwakilishi wake binafsi ameeleza kuwa siku ambazo amechelewa ni 45 pekee kwa kuwa siku 30 za mwanzo zilikuwa katika muda wa ruhusa kisheria wa kufungua mgogoro. Kama kanuni ya 10(1) ya T.L.S Na. 64 la mwaka 2007 ilivyoelekeza, mwakilishi wa mleta maombi ameielezea kanuni hiyo tofauti kwani yenyewe inaelekeza kuwa siku zitaanza kuhesabiwa tokea siku ambayo mwajiriwa amefahamu kuwa ameachishwa kazi. Kwa mantiki hiyo inaonyesha bayana kuwa mleta maombi alifikisha maombi ya mgogoro wake wa kazi akiwa nje ya muda uliowekwa kisheria.

Katika shauri la **Ramadhani J. Kihwani Vs. Tazara**, Civil Application Na. 401/18 ya mwaka 2018, Mahakama ya Rufani ya Tanzania – Dar es Salaam linaeleza kuwa ili kuongezewa muda; mleta maombi anawajibika kueleza sababu ya kuchelewa kwake katika kila siku moja aliyochelewa; kuwa: -

*"For the foregoing reasons, I find and hold that the applicant has not explained away every day of delay to warrant the Court exercise its discretion to grant the enlargement sought"*

Ikimaanisha

*"Kwa sababu zilizotangulia, naona na kushikilia kuwa mwombaji hajaeleza kila siku ya kuchelewa kuihakikishia Mahakama kutumia busara yake kutoa ongezeko la muda linaloombwa"*

Mleta maombi kupitia mwakilishi wake binafsi alieleza sababu ya kuchelewa kwake ni kuwa baada ya mgogoro wa kazi uliotokea tarehe 22/03/2022 tarehe 30/03/2022 alisafiri kuelekea Moshi kwa ajili ya kumuuguza mama yake. Hapa inaonyesha kuwa siku za tarehe 23/03/2022 hadi 29/03/2022 zikiwa ni jumla ya siku 6 mleta maombi hajazielezea nini kilifanya asifungue mgogoro wake katika siku hizo kabla ya kusafiri kwenda huko Moshi anakodai alikwenda. Katika kesi ya **Tanzania Fish Processors Limited V. Eusto K. Ntagalinda**, Maombi ya Madai Na. 41/08 of 2018, Mahakama ya Rufaa ya Tanzania - Mwanza ilielekeza kwa mleta maombi kuweza kuelezea siku zote alizochelewa. Katika shauri hili mleta maombi kupitia mwakilishi wake binafsi hajaweza kuelezea siku hizo 6 za mawanzo.

Pamoja na hayo, mleta maombi pia alieleza kuwa tarehe 30/03/2022 alienda Moshi na kukaa huko hadi tarehe 25/05/2022 kumuuguza mama yake na ili kuthibitisha hayo alifikisha Tume vielelezo vya tiketi za basi. Katika shauri la **Finca Tanzania Limited Vs. Hassan Lolila**, Civil Application Na. 165/18 of 2021, Mahakama ya Rufaa ya Tanzania – Dar

es Salaam, imeeleza kuwa Ni jambo la kawaida kwamba, masuala ya afya, mara nyingi, si chaguo la mwanadamu na hayawezi kuwekwa kando na wala mtu yeyote hawezi kulaumiwa yanapojitokeza. Hata hivyo ili kuyathibitisha ilisisitiza umuhimu wa kuwasilisha nyaraka zinazohusiana na matibabu hayo.

Hii ikimaanisha kuwa katika shauri lililorejewa kielelezo cha risiti ya matibabu kilitolewa kama kielelezo ili kuthibitisha ugonjwa wa mleta maombi uliosababisha kutokufika Mahakamani. Katika shauri hili mleta maombi hakuwasilisha katika Tume nyaraka zozote za matibabu wala kielelezo chochote cha kuweza kuthibitisha ugonjwa wa mama yake ili kuweza kuweza kuthibitisha uchelewaji wake. Kifungu cha 110(1) cha Sheria ya Ushahidi [Sura ya 6 Marejeo ya Mwaka 2022] inaeleza kuwa anayetoa dai fulani lazima athibitishe.

Uchambuzi huo wa hapo juu unaifanya Mahakama hii kuona ya kuwa mleta maombi ameshindwa kutoa sababu za msingi za kufanya aweze kupewa muda wa nyongeza katika kufungua shauri la mgogoro wa kazi.

Mleta maombi pia ameongelea suala la ubatili wa kisheria, kwamba kufukuzwa kazi bila kusikilizwa ni ubatili ambao unatakiwa kuishawishi

mahakama katika kuongeza muda ili ubatili huo uweze kushughulikiwa na mahakama. Ni kweli kuwa swala la ubatili linahesabiwa ni sababu tosha la kuongeza muda hata kama mleta maombi hakuelezea ipasavyo sababu ya kuchelewa kwake (**Athuman Ntandu na mwenzake dhidi ya Dustan Peter Rima (as an administrator of the estate of the late Peter Joseph Rima (ilivyorejelewa na Mwakilishi wa Mleta Maombi hapo juu)**. Lakini ubatili huo unatakiwa kuwa dhahiri katika mwenendo wa shauri linalotakiwa kuletwa mahakama. Katika kesi yetu hii hakuna shauri lolote lililokwisha letwa mahakamani ambapo mahakama ingeweza kuona ubatili huo ukiwa dhahiri kwenye mwenendo na maamuzi ya Mahakama ya chini au Tume. Ubatili huu haihusishi kitu ambacho kiko nje ya mashauri kama matendo ya mwajiri anayodai mleta maombi. Kwa mantiki hiyo, mahakama inakosa pa kushikilia kuhusiana na ubatili unaodaiwa na mleta maombi ili kumuongezea muda.

Mahakama hii baada ya kupitia maombi haya inaona kwamba maombi haya hayana mashiko kwa mleta maombi kushindwa kuelezea na kuthibitisha siku zote alizochelewa kufungua shauri na pia kushindwa kuonyesha ubatili wa kisheria inayweza kuchukuliwa kama sababu ya kuongezewa muda. Hivyo basi, mahakama hii inasimamia uamuzi wa

Tume na kwakuwa hili ni shauri la mgogoro wa kikazi, kila upande utajilipia ghalama zake.

MAHAKAMA KUU YA TANZANIA (The High Court of Tanzania) (Labour Division) DIVISHENI YA MAHAKAMA YA KAZI

**M. P. OPIYO,**

**JUDGE**

**25/4/2023**